

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ مَأْمُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَخْفَفُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفْتُ  
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يُمْكِنْنَهُمْ دِينُهُمُ الَّذِي أَرْتَهُمْ فَمَمْ لَيَبْدَأُهُمْ مِنْ بَعْدِ حَوْقَنِهِمْ أَمْ  
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئاً وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّافِرُونَ



Toleo Na: 01 / 1444 H

Ijumaa, 28 Muharram 1444 H

26/08/2022 M

### Taarifa kwa Vyombo vya Habari

#### Pendekezo la Kupiga Marufuku Hijab ni Tangazo la Vita dhidi ya Jamii ya Kiislamu (Imetafsiriwa)

Serikali mbalimbali za Denmark kwa muda mrefu zimefuata sera ya chuki dhidi ya Uislamu ilio dhihirishwa kwa sheria zinazolenga maadili na mfumo wa maisha wa Kiislamu. Serikali ya sasa inataka kupiga hatua kubwa mbele katika mapambano yake ya kidhalimu ya kuwaoanisha kwa nguvu Waislamu nchini Denmark.

Kupitia tume iliyoundwa na serikali, inayoongozwa na Meya wa Kidemokrasia ya Kijamii, na ambayo wanachama wake wengine wanajumuisha watu wasio na uwezo wanaochukia Uislamu, imechagua kukabiliana na marufuku ya hijab ya Kiislamu katika shule za msingi na sekondari.

Marufuku kama hiyo haiwezi kueleweka kuwa kitu chengine isipokuwa tangazo la wazi la vita dhidi ya umma wa Kiislamu. Inajulikana vyema nchini Denmark - na pia kote ulimwenguni - kwamba hijab ni faradhi kubwa ya Kiislamu. Fauka ya hayo, hijab imekuwa ni nembo ya kitambulisho cha Kiislamu, na inadhihirisha maadili matukufu kama vile adabu, uongofu na hadhi ya kuheshimika ya wanawake katika Uislamu. Haya ni maadili madhubuti ya Kiislamu, ambayo serikali ya Denmark tayari inapambana nayo vikali.

Kwa hoja ya "kupambana na udhibiti wa kijamii", udhibiti zaidi wa serikali wa Waislamu unatakwa na serikali kupitia kuwavua nguo kwa lazima wasichana wa Kiislamu na kuongezeka kwa ufuatiliaji wa familia za Kiislamu. Vitendo ambavyo haviko mbali na kufanana na sera ya kibabe ya utawala wa China dhidi ya Waislamu wa Uyghur.

Kuwavua nguo kwa kulazimishwa wasichana wa Kiislamu, hata hivyo, kutafichua tu ubaya wa mfumo wa kidemokrasia uliojengeka kwa dhuluma-ya-idadi ya wengi na kufilisika kwa maadili huria ya uhuru. Katiba ya Denmark, ambayo wanasiasa mara nyingi huwataka Waislamu kula kiapo cha utiifu, inahujumiwa na wao wenywewe.

Katika ugumba wa nguvu za kiroho mbele ya fikra za ushawishi za Uislamu na maadili ya kweli, walini wa demokrasia wamechagua kuvunja nguzo zinazoimarisha msingi wa jamii ya Denmark. Katika kutapatapa kwao kuwatiisha Waislamu, wanapigilia misumari ya mwisho kwenye jeneza la demokrasia.

Wanasiasiha hao wameshindwa kuwakinaisha wasichana na wanawake wa Kiislamu kwamba mtazamo mchafu wa thaqa ya Kimagharibi kuhusu wanawake na usherati ndio njia ya maisha huru na yenye furaha. Kwa hivyo, wanakimbilia kuhamisha na kulazimisha. Lakini wasichana wa Kiislamu wanasisitiza kuishi maisha ya kimaadili na kuvaa kwa heshima, huku wakizidi kuijeweka mbali na mtazamo duni wa Kimagharibi wa wanawake.

Tunataka kuweka wazi kwa serikali ya Denmark na umma kwamba Waislamu kamwe, hawatakubali kupigwa marufuku kwa hijabu.

Tutapambana na kila kitu tulicho nacho ili kuzuia marufuku kama hii kuwa uhalisia. Tutapigania haki yetu ya kuvaa kama Muumba wetu alivyotuamuru, na jukumu letu la kuwalinda dada na binti zetu wapendwa.

Wasichana na wanawake wa Kiislamu lazima waweze kuvaliwa hijab zao kwa fahari kila mahali: shulen, sehemu za kazi na katika maeneo ya umma. Wanasiisa wanaochukia Uislamu bado hawaonekani kufahamu kwamba tutapigania hadi pumzi zetu za mwisho kwa ajili ya kitambulisho na maadili yetu.

Sisi katika Hizb ut Tahrir tunawalingania Waislamu wote kusimama pamoja, kufanya kazi pamoja na kupigana bila kuchoka kwa namna ya Kiislamu hadi mwisho kwa ajili ya jukumu hili tukufu la Kiislamu ambalo hatutaliacha kamwe.

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir  
Denmark